

HALMASHAURI YA MJI

IFAKARA



KILIMO CHA MBOGA

MJINI



KILIMO CHA MBOGA MJINI

UTANGULIZI

Ongezeko la watu mjini na kupanuka kwa Mji vina-sababisha ongezeko la mahitaji ya chakula ma-radufu. Ili kukidhi mahitaji ya chakula kwa wakazi inabidi kilimo cha mjini kipewe kipaumbele.

Mboga za majani ni muhimu sana kwa afya ya bi-nadamu, zinaongeza vitamin A na C mwilini. Hata hivyo pamoja na umuhimu wake watu wengi waishio mjini wamekuwa wakishindwa kulima mboga kuto-kana na uhaba wa maeneo. Kulima kwenye vyombo kunatatua tatizo hilo.

VYOMBO VINAVYOTUMIKA KUOTESHA MBOGA.

Vyombo vibovu, viroba, creti za mbao, mifuko ya nailoni, mapipa mabovu, ndoo, makapu, makopo, matenga na magunia.

Mboga zikiwa zimepandwa katika mifuko ya plastiki na kiroba



UTAYARISHAJI WA VIFAA VYA KUPANDIA

Hakikisha vifaa vyote vimetobolewa upande wa chini ili kuwezesha maji yanayomwagiliwa kutoka badala ya kutuama kuozeza mizizi isipokuwa matenga yana nafasi ya kutosha.

UDONGO WA KUPANDIA.

Udongo unaofaa kwa kilimo hiki ni ule unaopitisha maji yaani tifutifu na siyo mfinyanzi.

Kwa kuwa maeneo yaliyo mengi ni mchanga chanya udongo pamoja na mbolea ya samadi iliyooza au tumia mboji, ili udongo uweze kushikana na kuhifadhi unyevunyevu kwa mda mrefu. Mwangilia udongo kabla ya kupanda. Viwango vya kuchanganywa udongo na mbolea:

Udongo vipimo vinne (4)

Mbolea vipimo viwili (2)

Mchanga kipimo kimoja (1)

Ina maana uwiano ni 4:2:1

NJIA ZA KUPANDA MBOGA

Mboga za kwenye vyombo hupandwa kwa njia tatu, nazo ni:-

Kupanda mbegu moja kwa moja ambazo husambazwa kwenye chombo kwa mfano mchicha, karotina kadhalika.

Kupandikiza miche kutoka kitaluni kwa mfano bilinganya, nyanya, sukumawiki n.k. Wakati muafaka wa kupandikiza miche ni jioni.

Kupandakwa kutumia vikonyo mfano matembele.

UTUNZAJI.

Umwagiliaji maji kila siku asubuhi na jioni, maji mboga itakapovunwa.

UDHIBITI WA WADUDU NA MAGONJWA.

Wadudu na magonjwa yanadhhibitiwa na madawa kama vile mwarobaini, kitunguu swaumu n.k.

FAIDA ZA KUTUMIA VYOMBO.

Ni rahisi kuhudumia.


Hupandwa hata magorofani kama maua.

Ni rahisi kupata mboga wakati wote

Mboga zinakuwa safi kwani kunakuwa na maji wa kutumia maji safi.

Maji yanayotumika ni kidogo na rahisi kutumia kwa kutumia chupa.

Ni rahisi kuhudumia kwa sababu ya ueneo



Kimetayarishwa na:

IDARA YA KILIMO, UMWAGILIAJI NA USHIRIKI

HALMASHAURI YA MJI IFAKARA

S.L.P. 433,

IFAKARA

TEL: +255 23 293 4212

FAX: +255 23 293 4212

TOVUTI www.ifakaradc.go.tz

BARUA PEPE.info@ifakaradc.go.tz

